# MLIMA WA ELIMU



## ELIMU YA UFALME DHIDI YA ELIMU YA WAKALDAYO

JAMES KALEKWA

# MLIMA WA ELIMU:

*Elimu ya Ufalme dhidi ya elimu ya Wakaldayo*

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo


Uelewa kuhusu Elimu ........ 4

Mfano 1: Elimu ya Wakaldayo ........ 6

Mfano 2: Elimu chini ya Gamalieli ........ 8

Mfano #3: Elimu ya Waganga ........ 13

Mfano #4: Elimu ya Utafiti katika kueneza Injili ........ 19

Kuhusu Mwandishi: ........ 26

Kuhusu New Vine Church: ........ 26

Mawasiliano na Mwandishi: ........ 27

## Uelewa kuhusu Elimu

- Elimu ni mjumuiko wa taarifa na maarifa ambayo huhamishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kizazi kingine.

- Elimu ipo ili kuwajengea watu uwezo kuyakabili mazingira yao; kutumia rasilimali na nafasi ambazo Mungu amewawekea ili kupata ustawi.

- Elimu huwafinyanga/huwatengeneza watu kuwa vile tunavyowaona leo. Yaani, vile mtu anavyoonekana na kutenda leo ni matokeo ya elimu aliyoipata na inayotenda kazi ndani yake.

- Elimu huwatengeneza watu kuwa vile inavyotaka wawe. Elimu imeundwa kufinyanga watu kutoshea kwenye mfumo na utendaji wa aina fulani. Kwa hiyo, mtu anapoingia kwenye mkondo fulani wa elimu ni vigumu kuchagua kutenda nje ya mkondo huo.

- Elimu ni kiwanda kinachowatengeneza watu kwa kuwapa UELEWA/UFIKIRI/MTAZAMO (Paradigms). Mtazamo ni kama miwani ambayo mtu huitumia kuyaona, kuyaelewa,

kuyatafsiri maisha na kuchukua hatua kutokea kwenye uelewa huo.

- Anayeshikilia MLIMA WA ELIMU ameshikilia maisha ya kizazi kilichopo na kijacho.

**Aina za elimu:**

1. Elimu rasmi: hii ni elimu amabayo hutolewa kwa utaratibu ulio rasimishwa. Kama vile mitaala, madarasa/madaraja, upimaji [mitihani] na matokeo.
2. Elimu isiyo rasmi: hii ni elimu ambayo hutolewa pasipo mfumo ulio rasimishwa.

Hata hivyo, mimi, ni muumini wa elimu jumuishi [holistic], inayogusa nyanja zote za maisha, kuwajengea watu uwezo wa kuyaelewa mambo na kuinuka juu ya changamoto zao. Mungu alikusudia tuyatawale mazingira yetu kwa viwekezo alivyoweka ndani yetu. Na tufanyapo hivyo, Yeye hutukuzwa. Na kwa maoni yangu, elimu inapaswa kumuelekeza mwanadamu kuwa hivyo.

Sehemu zinazofuata za kitabu hiki, nitafundisha kwa kurejelea mifano kadhaa kwenye Maandiko Matakatifu kuonyesha mawanda ya mlima wa elimu.

## Mfano 1: Elimu ya Wakaldayo

"3. Mfalme [Nebukadreza] akamwambia Ashpenzai, mkuu wa matowashi wake, awalete baadhi ya wana wa Israeli, wa uzao wa kifalme, na wa uzao wa kiungwana. 4. Vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, **wajuzi wa hekima, werevu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu**, **watakaoweza kusimama katika jumba la mfalme**; tena alimwambia **awafundishe elimu ya Wakaldayo,** na lugha yao."

Danieli 1:3-4 SUV

Kutokea kwenye andiko hilo utaona mambo yafuatayo:

- ✓ Kuna vigezo vingi vilitumika kuwapata vijana hawa [vetting] kutoka miongoni mwa vijana wengi wa Yuda waliochukuliwa uhamishoni Babeli; kigezo kimojawapo ni ELIMU. Ni rahisi mtu mwenye elimu, kuongezeka kielimu.

- ✓ Lengo la kuwapata vijana hao ni ili "wasimame" katika jumba la mfalme – kusimama siyo jambo la kimwili kama vile walinzi bali ni kutenda kazi ili kuuwezesha ufalme wa Nebukadreza usogee mbele. Biblia ya lugha ya kiingereza tafsiri ya Amplified Bible inasomeka hivi: *"…and quick to*

*understand, competent to stand [in the presence of the king]* ***and be able to serve in the king's palace****…"*

- ✓ Kabla hawajaingia "kusimama" kwenye jumba la mfalme kuna kitu cha nyongeza kinatakiwa kufanyika – wafundishwe ***elimu ya Wakaldayo*** na ***lugha yao*** [mfumo wa mawasiliano]. Tafsiri ya amplified inasema "literature" mahala pa "elimu". Unaweza ukaelewa ni elimu iliyo kwenye machapisho. Kabla hatujaenda mbali na wazo hili, ni vyema kufahamu ya kwamba hawa vijana walikuwa na elimu tayari. Kwa nini tena kuwafundisha elimu?
    - ➢ Wamefundishwa/wana Elimu ya Israeli; Israeli ni taifa lenye mahusiano ya kibanfsi na Mungu, Yehova (kwenye maisha yao yote, elimu ikiwemo kuna kigezo cha Mungu "the God factor" – Rejea torati. Iligusa kila eneo na nyanja ya kimaisha); – mfumo wa elimu ya Israeli uliwawezesha kutenda kazi na kuzalisha matokeo wenye mfumo wa Israeli, uliokuwa na Mungu ndani yake.
    - ➢ Ilikuwa ni lazima wabadilishiwe "mitazamo/uelewa/paradigms" ili

watende kazi kwenye mfumo wa kibabeli chini ya mfalme Nebukadreza, wenye miungu ndani yake.

- ✓ Hawa vijana walimchezea shere [played games] shetani – kumbe hawakufuta elimu yao ya Kiebrania – yenye uwepo wa kigezo cha Mungu kwenye utendaji na utekelezaji. Walikuwa kimya ili wasigundulike mpaka walipokalia nafasi!

- ✓ Hii inadhihirika hasa walipopanda kwenye jumba la mfalme [Danieli alikuwa ni sehemu ya wenye hekima wa Babeli (advisors) – waliendelea kuomba, kumwabudu Mungu, Yehova.

- ✓ Tunajua madhara waliyopeleka kwenye ufalme wa giza. Ni elimu ya kiungu ilikuwa kazini kuupindua mfumo wa elimu ya miungu.

## Mfano 2: Elimu chini ya Gamalieli

"Mimi ni mtu wa Kiyahudi, nalizaliwa Tarso, mji wa Kilkia, **ila nililelewa katika mji huu, miguuni pa Gamalieli, nikafundishwa sheria ya baba zetu kwa**

**usahihi**, nikawa mtu wa jitihada kwa Mungu kama ninyi nyote mlivyo leo hivi."

Matendo ya Mitume 22:3 SUV

**Huyu Gamalieli ni nani?**

"Lakini mtu mmoja, **Farisayo**, jina lake Gamalieli, **mwalimu wa torati**, **mwenye kuheshimiwa na watu wote**, akasimama katika baraza akaamuru mitume wawekwe nje kitambo kidogo."

Matendo ya Mitume 5:3 SUV

Paulo asingemrejelea Gamalieli kwenye utetezi wake dhidi ya mashitaka yaliyokuwa yanamkabili kama mtu huyu angekuwa si wa umuhimu wowote.

Kuna walimu wanaheshimika kwenye nyanja fulani za kitaaluma. Kiasi kwamba ukiwataja, heshima yao inakufunika na wewe. Ndivyo ilivyokuwa kwenye muktadha huu.

Paulo anasimulia matokeo ya kuwa mwanafunzi wa Gamalieli ni "...kuwa mtu wa jitihada kwa Mungu...". Mimi nimekuwa mwanafunzi wa walimu kadhaa kwenye elimu ya juu. Ninaweza kuwa shahidi kwenye hili. Kuna walimu wakikufundisha ni kwa sababu tu wanalipwa mshahara. Halafu kuna walimu wakikufundisha unakua (you become). Wanaweza wasikutaje kwa jina na kukuelekeza cha kufanya.

Lakini, namna yao ya kufundisha inakuhimiza uwe kile kinachofundishwa.

Mzee Gmalieli alikuwa ni aina hii ya mwalimu. Anafinyanga watu!

**Akawa mtu wa jitihada?**

Hebu fuatilia maandiko yafuatayo yanayoidhihirisha jitihada/juhudi ya ndugu Sauli, mwanafunzi wa Mzee Gamalieli.

Matendo ya Mitume 9:1-2 SUV
“Lakini Sauli, akazidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana, akamwendea Kuhani Mkuu, 2. Akataka ampe barua za kuenda Dameskizilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake, awafunge na kuwaleta Yerusalemu.”

Galatia 1:13-14
“Maana mmesikia habari za mwenendo wangu, zamani katika dini ya Kiyahudi, kwamba naliliudhi kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu 14. Nami naliendelea katika dini ya Kiyahudi kuliko wengi

walio hirimu zangu katika kabila yangu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu."

Filipi 3:6 SUV
"kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi Kanisa, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia."

- Nini kilizalisha mtazamo huo wa chuki dhidi ya kanisa ndani ya Paulo? – elimu!
- Nini kilizalisha shauku/usongo fulani wa kulifuta kanisa kwenye uso wa nchi? – elimu!
- Hata wanaomshtaki anawaelewa ya kwamba "jitihada waliyonayo hivi leo" ni matokeo ya elimu!

Kuna aina fulani ya elimu ukipokea, huwezi kuepuka kuwa aina fulani ya mtu. Si unajua kuna aina fulani ya madarasa ambayo mtu akiingia ndani yake inazaliwa chuki na uhasama dhidi ya mwili wa Kristo duniani, kanisa. Ni elimu tu! Elimu huzalisha himizo na hamasa ndani ya wanafunzi la kuwa aina fulani ya watu.

**Elimu ya nadharia na vitendo:**

Kwenye uga wa elimu, kuna upande wa ***elimu ya nadharia***. Elimu nyingi inayotolewa ngazi za juu [uzamili na uzamivu] huwa ni juu ya dhana

(concepts) na nadharia (theiories) na namna gani hujaribu kuufafanua uhalisia (realities) unaoendelea kwenye jamii. Wakufunzi wengi wa elimu kwenye ngazi hii huwa si watendaji sana ikija kwenye uhalisia. Wanaweza kuchambua nadharia, ulezea dhana na kujenga hoja tu. Mzee Gamalieli alikuwa kwenye daraja hili.

Upande wa pili kuna ***elimu ya utendaji***. Hii hutolewa kwenye vyuo vya “polytechnique”. Hivi hujikita kuzalisha watu wanaoweza kutafsiri nadharia kuja kwenye matendo na uhalisia wa siku kwa siku kwenye jamii. Hawa ni watendaji wa elimu (practitioners) fulani. Watu wengi wa kwenye kundi hili hawana ujuzi wa nadharia na dhana nyingi sana. Wanajua kutekeleza tu.

Nimeanza na utangulizi huo ili nikuonyeshe namna ambavyo Sauli alijifunza nadharia kwa Gamalieli (ambaye hakuwa mtekelezaji wa maudhi kwa kanisa) kwa upande mmoja; na alijifunza utendaji na utekelezaji kwa kundi la “practitioners” wa maudhi kwa kanisa. Kundi hili lilifahamika kama mashahidi.

Na hivyo ndivyo Sauli alivyofinyangwa kielimu.

Hebu tutazame neno la Kristo linasemaje.

Matendo ya Mitume 7:58

“Wakamtoa [Stefano] nje ya mji, wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi **wakaweka nguo zao miguuni pa kijana mmoja aliyeitwa Sauli**.”

Kwa hiyo mtazamo wa Paulo wa kikatili na uuaji ni muunganiko wa mafundisho ya sheria kinadharia [theoretical] ya Gamalieli na ya watendakazi [practitioners] ya Mafarisayo wafia dini almaarufu mashahidi au mahuru.

Matendo ya Mitume 6:9

“Lakini baadhi ya watu wa sinagogi lililoitwa sinagogi la Mahuru, na la Wakirene, na la Waiskanderia, na la wale wa Kilikia na Asia, wakaondoka kujadiliana na Stefano.”

Kwenye hili kundi la Mahuru walikuwemo Wakirene, Waiskanderia, Wakilkia, WaAsia.

Hawa ndiyo waliomuonyesha kwa vitendo na mna ya kuitetea dini ya Mungu; dini ya Kiyahudi; dini ya baba zao. Sauli ni zao la elimu.

## Mfano #3: Elimu ya Waganga

Kuna elimu ambayo iliongoza maisha ya watu wakati fulani kwenye jiji kubwa la wakati wake, jiji la Efeso. Usisahau kile nilichokitambulisha kwako ya kwamba, elimu humuwezesha mtu kuzalisha matokeo ya kimaisha na kuweza kutenda kwenye mfumo fulani.

Sasa, kwenye jiji la Efeso, mahalai ambapo kulikuwa na shughuli nyingi za kimaisha zikiendelea. Kumbe, ulihitaji uwa na elimu fulani ili ujipatie kipande chako kwenye ardhi ya maisha. Na kuna watu, walijibidiisha kwenye elimu ya kiganga.

Hebu tusome maandiko yanasemaje:

Matendo ya Mitume 19:19-20

“19. Na watu wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga **wakakusanya vitabu vyao**, wakavichoma moto mbele ya watu wote; wakafanya hesabu ya thamani yake, wakaona ya kwamba yapata fedha hamsini elfu 20. Hivyo ndivyo **neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu**.”

Ukiona walikuwa na vitabu lakini walikuwa wanatumia mambo ya uganga, basi uwe na uhakika walikuwa wanasoma. Ni kama vitabu vya mwongozo wa mapishi “recipies”. Ukitaka kufanikiwa kwenye biashara kwa namna ya uganga fanya yafutayo; Au ukitaka kupata mpenyo wa kifedha kwa namna ya kiganga zingatia yafuatayo; Au namna ya kuwa na ndoa, kupata uzao n.k. Kitu muhimu nataka uone ni kwamba njia za uganga hazikuwa za hovyo hovyo, bali zilikuwa na elimu iliyoandikwa na kuratibiwa.

Ni vizuri ufahamu ya kwamba kama njia hizo zisingekuwa zinawaletea matokeo, wangekuwa

wameachana nazo kitambo. Kumbuka, watu wengi maishani wanataka vitu vinavyotenda kazi na kuleta matokeo (pragmatic). Hivyo, wasingeendelea kukumbatia kitu ambacho hakina tija kwao.

Sasa, kufikia mahali ambapo watu wanaoishi kwa kutumia elimu ya kiganga kufanya maamuzi ya kuchoma vitabu vyao. Ni kama walikuwa wanachoma maisha yao; wanachoma hatima zao. Ujue kuna elimu kubwa sana ambayo wameipokea na wamejihakikisha pasipo kivuli cha mashaka.

Hebu fuatana na mimi kugundua mchakatao uliotumika kupasua elimu ya kiganga kwenye maisha ya watu:

Kinachotokea hapo ni matokeo ya 19:8-11

“8. Akaingia ndani ya Sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu 9. Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakaitukana ile Njia mbele ya mkutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akohiajana na watu kila siku katika darasa la mtu mmoja, jina lake Tirano. 10. Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani 11.Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida.”

**Uwekezaji wa muda:**

- ✓ Mkutano wa miezi mitatu; sawasawa na siku 90 mtume Paulo anaongea na wasioamini. Na anaongea nao kuhusu injili.
- ✓ Wengine walikataa na kuitukana “Njia ile” – yaani, imani ndani ya Kristo. Baada ya uwekezaji wa siku 90.
- ✓ Yakafuatia mafundisho/semina ya miaka 2. Fikiria mnahudhuria mafundisho kwa miaka miwili.
- ✓ Ni muda wa kozi ya diploma /au baadhi ya shahada.

**Mahojiano:**

- ✓ Mtindo alioutumia mtume Paulo kwenye jamii ya Efeso; mahali ambapo elimu ya kiganga ilikuwa imeweka ngome kwenye mji, mioyo na maisha ya watu kwa ujumla.
- ✓ Ndani ya siku 90 alikuwa akihojiana na wasioamini; ndani ya miaka 2 alikuwa akihojiana na waamini.
- ✓ Hii ni kama mjadala au mdahalo. Mahali ambapo si yeye tu alikuwa anazungumza. Lakini alipata wasaa kujua kinachoendelea kwenye mioyo ya watu kwa njia ya mjadala.

**Msukumo wa ndani:**

- ✓ Kulikuwa na aina fulani ya nia na nguvu nyuma ya ufundishaji wa mtume Paulo.
- ✓ Alinena kwa ushujaa (boldiness); hakuwa dhaifu (mlaini) au mlegevu kwenye uwasilishaji wake. Alijua anapambana na ngome za uganga kwenye ngazi ya elimu ambayo imeshikilia fahamu za watu.
- ✓ Akiwavuta katika mambo ya ufalme. Lengo lilikuwa ni kuwavuta waingie kwenye ufalme.

Baba yangu wa kiroho na Mchungaji wangu, mwangalizi wa makanisa ya New Vine ulimwengu, Pastor Goodluck Kyara alinifundisha siku za mwanzoni kabisa za utumishi. Ya kwamba mimi si mhamasishaji au muwasilishaji wa habari. Bali ni mtumishi wa Mungu. Hivyo, ninapaswa kuhudumu kwa namna ambayo maisha ya watu yatapokea mgeuko (Son, don't just inform, transform).

Matokeo:

Baada ya kuona uwekezaji aliofanya mtume Paulo wa kung'oa elimu ya kiganga kwenye fahamu za watu. Biblia inasema kuna **miujiza ya kupita kawaida** ikafanyika (Matendo ya Mitume 19:11-12). Nilishtuka siku neno hili liliponifunukia kwa nguvu; nikagundua kuna miujiza ya kawaida na miujiza ya kupita kawaida. Hii ilikuwa ni uthibitisho wa nguvu wa kile

alichokifundisha kwa miaka miwili na zaidi. Kristo ni hekima ya Mungu na ishara; wanaotafuta hekima na wanaotafuta ishara, wote wanajibiwa!

Na hitimisho la aina hii ya uwekezaji wa elimu ya kiungu lilikuwa ni kukusanya vitabu vya kiganga na kuvichoma moto mbele ya watu wote (Matendo ya Mitume 19:19). Hapa ndipo ngome za elimu ya kiganga zilianguka rasmi kwenye fahamu za watu. Wakaamua, kwa hiyari yao wenyewe kuachana (divorce) kabisa na elimu ya kiganga na kufuta kumbukumbu na rejea ya namna yoyote. Ni sawa na kusema, hawatarudi tena kwenye elimu hiyo. Hawana vitabu, machapisho wala mahali pa kurejea.

**Changamoto:**

Si nia yangu kwenye kitabu hiki kwenda kwenye taarifa za ndani za gharama ya vitabu vilivyochomwa. Lakini ninataka kuwasilisha changamoto mbele yako msomaji wangu. Hebu fanya utafiti kujua vitabu vya thamani ya "fedha hamsini elfu" kwa sasa vingekuwa na gharama kiasi gani?

Note: fedha hapa haimaanishi hela bali material (silver) – kwa nyakati hizo kulikuwa na drakma na dinari, shekel.

## Mfano #4: Elimu ya Utafiti katika kueneza Injili

"Luka **yule tabibu** mpendwa, na Dema, wanawasalimu." Wakolosai 4:14

"Luke, the beloved **physician**, and Demas, greet you." (King James Version)

"Greetings also from Demas and our beloved friend Luke, **the doctor**." (Holy: Easy-to-Read Version)

Kwenye kipengele hiki ninataka kukuletea uelewa mbele yako kuhusiana na msomi wa elimu ya tiba (tabibu) aitwaye Luka. Kama hufahamu tabibu ni nani, ni daktari!

Huyu ndiye mwandishi wa injili ya Luka na kitabu cha Matendo ya Mitume. Kiasi kwamba baadhi ya wanatheolojia wamtajapo Dokta Luka husema mchango wake kwenye Biblia ni uandishi wa kitabu cha "Luka-Matendo".

Injili ya Luka iliandikwa kama taarifa ya utafiti (research report). Na mkusudiwa au msomaji mkubwa wa taarifa hii ya utafiti alikuwa "Theofilo mtukufu".

Ili kusaidiwa kuelewa kwa urahisi kile ambacho nitakionyesha hapa. Ninaambatanisha mistari mine ya kwanza ya kitabu cha Injili ya Luka.

*“1.Kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa taratibu habari za mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu. 2. Kama walivyotuhadhithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo, 3. Nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa utaratibu, Theofilo mtukufu, 4. Upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa.”* Luka 1:1-4 (SUV)

Kutokea kwenye andiko hili ninaomba tuambatane kutambua mambo kadhaa.

**Kuhusu mwandishi:**

Nimetumia sehemu ya kwanza ya kipengele hiki cha elimu ya utafiti katika kueneza injili, kumwelezea mwandishi. Jambo ambalo tunajua kwa hakika kutokea kwenye maandiko alikuwa ni tabibu/daktari wa kutibu.

**Mlengwa wa awali:**

Mwandishi wa injili ya Luka anamwandikia “Theofilo mtukufu”. Kwa ujumla wake, alimwandikia mtu wa heshima na hadhi kwenye jamii. Alikuwa ni nani haswa, Biblia haisemi. Hta hivyo heshima ya “Mtukufu” ukisoma Matendo ya Mitume 23:26 na 24:2 utamuona Feliki na ukisoma 26:25 utamuona

Festo wakitajwa kwa heshima hiyo. Hawa walikuwa ni maafisa kwenye serikali ya kirumi wakati huo. Kwa hiyo, inaweza kuwa sawa kuhitimisha ya kwamba Theofilo alikuwa ni afisa wa ngazi ya juu wa serikali ya kirumi. Hata hivyo kuna baadhi ya watheolojia humwelezea Theofilo ama alikuwa mtu tajiri mwenye fedha; AU kuhani wa dini ya kiyahudi AU mwanasheria.

Kwa matumizi ya kitabu hiki, ninapenda kumtazama Theofilo kama afisa wa serikali mwenye hadhi na heshima – mtukufu.

Ukisoma kwenye injili ya Luka, utagundua, mtu huyu aliokoka na kupata mafundisho ya “Waamini wapya” kutokea mahali fulani.

Hata hivyo, kwa sababu ya heshima na hadi yake inawezekana hakuwa na muda au muunganiko wa moja kwa moja na jamii ya waamini. Hakuwa anakusanyika pamoja na waamini ili kupata mwendelezo wa msingi wa mafundisho aliyopokea mwanzoni.

Huu mwanya “missing link” baina yake na jumuiya ya imani ulipeleka kuibuka kwa kundi la watu ambalo Daktari Luka analielezea “*Kwa kuwa watu wengi **wametia mikono kutunga kwa taratibu** habari za mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu.” Luka 1:1.* Kuna watu wakatia mikono kutunga habari za Yesu;

tena anasema walitunga “kwa taratibu”. Hii taratibu haimaanishi “kwa upole au polepole” bali neno la kiingereza linalotumika ni “systematic”, yaani kwa mpangilio na mtiririko maalum. Yaani, uongo na upotofu unapangiliwa vizuri.

**Kwanini?**

Usisahau ya kwamba Theofilo alikuwa mtukufu – afisa wa ngazi za juu kwenye serikali ya kirumi. Kwa hiyo, inawezekana waandishi wa uongo walitaka kujipatia fedha kwa kumuuzia tafiti za uongo; ama inawezekana walitaka kujipatia upendeleo fulani kwenye maswala ya serikali. Au ulikuwa ni mkakati wa wanasiasa wenzake kumrudisha kwenye “magenge” yao kwa kumtenga mbali na kanisa. Na njia ya kufanya hivyo ni kumlisha elimu ya kutunga.

**Lengo la uandishi:**

*“Upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa” Luka 1:4*

Daktari Luka anaandika ili kuyathibitisha yale ambayo mtukufu Theofilo alifundishwa awali. Na kufanya hivyo, kupangua uongo uliotungwa *systematically* na waandishi waliokuwa “wakimuuzia” vitabu Theofilo.

Ukusanyaji wa “data”:

*“Nimeona vema mimi nami, kwa kuwa **nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo**…” Luka 1:3*

Daktari Luka anaonyesha ya kwamba taarifa zake si za kutunga. Ni mambo ambayo ameyatafuta na kwa ujuzi wake wa kielimu alitafuta usahihi wa mambo. Msomaji, kama unafahamu kuhsiana na uliwengu wa taaluma na tafiti utakubaliana na mimi ya kwamba kitafiti, si kila taarifa ni sahihi; ni kweli yaweza kuwa taarifa lakini isiwe sahihi. Kinachoamua usahihi wa taarifa kwenye ulimwengu huu ni vyanzo vya taarifa. Na vyanzo ambavyo hupokelewa bila tashwishwi ni vyanzo vya msingi vya taarifa (Primary sources of data).

Kuhusiana na hili Daktari Luka anasema, “*Kama walivyotuhadhithia wale **waliokuwa mashahidi wenye kuyaona**, na **watumishi wa lile neno tokea mwanzo**” Luka 1:2*

Alijikusanyia taarifa kutoka kwa mashahidi wenye kuyaona (eye witnesses) na watumishi wa neno tokea mwanzo. Unahitaji nini kingine kuthibitisha uhalali wa taarifa alizokusanya daktari?

Kama ungependa kufahamu, kwa maoni yangu, huu ulikuwa ni utafiti uliotumia methodolojia “Qualitative” kwa sababu ya kuhadithiwa; yaani, alikusanya taarifa zenye maelezo ya kina, mafafanuzi,

masimulizi… kwa lugha ya kitafiti zaidi, inawezekana alifanya in-depht interviews, au Focused Group Discussions, au journaling au observations kwenye maeneo na watu waliohudumiwa na Yesu… inawezekana! Ninachotaka uone ni namna daktari Luka anaishughulisha elimu yake kwa ajili ya injili.

**Uandishi wa utafiti:**

*"…kukuandikia kwa utaratibu, Theofilo mtukufu,"*
***Luka 1:3b***

Baada ya kukusanya "data" na kuzichambua, daktari Luka anaandika kwa utaratibu. Ninajua umeshaelewa ni uandishi wenye mpangilio na mtiririko maalum – systematically!

Ili kupangua elimu ua uongo iliyopandikizwa systematically; lazima kuwasilisha injili systematically. Si kila mtu ana hiyo neema. Wapo akina daktari Luka. Kama wewe ni mmoja wao, chukua nafasi yako kwa nguvu.

Kwa muda nimekuwa nikimfuatiliwa mmoja wa watu wa muundo huu kwenye zama zetu, Dr. Ravi Zacharias (marehemu kwa sasa). Yeye na huduma aliyokuwa anaiongoza walibeba jukumu la kufikia

jamii ya wanataaluma wa vyuo vikuu. Mahali ambapo upagani na upinga Kristo unashamiri kwa wingi. Ilikuwa ikinishangaza mar azote kuona namna gani anatumia taaluma kumwinua Kristo kwenye mlima wa elimu.

**Taarifa ya ziada: tafiti hufadhiliwa**

Kwa wasiofahamu, tafiti nyingi unazosikia zimefanyika na matokeo yake kuanza kushirikishwa kwenye maeneo mbalimbali, huwa zinafadhiliwa. Mimi nimefanya tafiti mbalimbali na mashirika mbalimbali nikiwa kwenye madaraja tofauti: kama muandaaji wa utafiti, mkusanyaji wa taarifa (data collector), kama mchambuzi wa taarifa (data analyst), kama mwandishi wa taarifa ya utafiti (research report writer) na kama mpashanaji habari wa utafiti (dissemination). Nimeshuhudia wafadhili wa tafiti wenye uelekeo fulani wa kitaaluma, kisiasa, kiuchumi, kifalsafa. Na hiyo ina sauti juu ya yanayotokeza kama matokeo ya utafiti.

Tafiti nyingi na taarifa nyingi tunazozipokea na kuziheshimu kuwa ni za kitaaluma, uwe unajua au haujui, zinamsukumo nyuma yake. Na ni zaidi ya

msukumo wa wa kinadamu. Ni msukumo wa kiroho (spiritual influence).

Inahitajika mashujaa wainuke kutokea mlima Sayuni waweze kusimama kwenye mlima wa elimu na kumwinua Kristo Yesu hapo.

*"Tena waokozi watakwea juu ya mlima Sayuni ili kuuhukumu mlima wa Esau; na huo ufalme utakuwa ni mali ya BWANA."* **Obadia 1:21**

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila

nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja

kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764